# Ijue Sengerema

TOLEO NAMBA 01 OKTOBA HADI DISEMBA 2022

LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI CHA HALMASHAURI WA WILAYA YA SENGEREMA www.sengeremadc.go.tz Email: ded@sengeremadc.go.tz





# Bilioni 3.04 Zakamilisha Vyumba vya Madarasa 152

Jumla ya Shilingi Bilioni 3,040,000,000 za kitanzania zimekamilisha ujenzi wa vyumba 152 vya madarasa katika shule 31 za Sekondari zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.

Kukamiika kwa vyumba hivyo vya madarasa kutaisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kupunguza Msongamano wa wanafunzi na kuondoa tatizo la upungufu wa madarasa kwa shule za Sekondari.

Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema imejenga vyumba vipya 152 vya madarasa kwenye shule za sekondari 31 kwa gharama ya shilingi 3,040,000,000 fedha kutoka Serikali kuu.

Akikopeka Madarasa hayo, kwenye hafla fupi iliyofanyika Sekondari ya Nyampulukano, Mkuu wa Wilaya ya Sengerema Mhe. Senyi Ngaga amewaasa walimu na wanafunzi kuhakikisha wanaitunza vyema miundombinu hiyo ili iweze kudumu na kuleta manufaa kwa wote.



Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ndugu Mwita Waryuba akitoa taarifa ya ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa amesema, hadi kufikia tarehe 28 Disemba jumla ya vyumba 144 vilikuwa vimakamilika kati ya vyumba 152 sawa na asilimia 95.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema Mhe. Yanga Makaga amemshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za ujenzo wa vyumba hivyo kwani kumesaidia kutokusumbua wananchi kuchangia shughuli za ujenzi wa madarasa hayo.

Kukamilika kwa ujenzi wa madarsa hayo ulioanza mwezi Oktoba 2022 kunaifanya Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kumaliza tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa kwa shule za Sekondari.



# DC Atoa Onyo Watakaopuuzia Kidato Cha Kwanza

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema Mhe. Senyi Ngaga ametoa onyo kali kwa wazazi au walezi watakao shindwa kuwapeleka watoto wao kujiunga na kidato cha kwanza mwezi Januari 2023 kwani Serikali imejenga madarasa ya kutosha katika shule za Sekondari.

Mkuu wa Wilaya ametoa onyo hilo leo Disemba 28, 2022 wakati wa hafla ya ya makabidhiano ya ujenzi wa vyumba 152 vya madarasa ya Sekondari iliyofanyika Sekondari ya Nyampulukano katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.

Mkuu wa Wilaya amesema hivi sasa Serikali imejenga na kuweka miundombinu ya kutosha katika shule za sekondari hivyo hakuna sababu ya wazazi kushindwa kuwapeleka watoto kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza mwezi Januari 2023.

"Mtoto ambaye amepangiwa kwenda kidato cha kwanza mwaka huu ni lazima aende, mtoto asipoenda shule wakati madarasa tena yenye madawati yameandaliwa huo ni uhujumu uchumi na mwaka huu lazima tutoe mfano kwa wazazi wote watakao kaidi kupeleka watoto kidato cha kwanza na ninamanisha katika hili" amesisitiza Mkuu wa Wilaya.

Mhe. Mkuu wa Wilaya mbali na kuipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kwa kukamilisha ujenzi wa vyumba hivyo kwa wakati, amewaomba wadau mbalimbali kujitokeza kuwasaidia watoto wenye uhitaji waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza kwa kuwasaidia baadhi ya mahitaji ikiwemo madaftari na mahitaji mengine ya mhimu ili wote waweze kuanza masomo kwa wakati.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema Mhe. Yanga Makaga amepongeza Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha hizo kwani kupitia fedha hizo zimekamilisha ujenzi wa vyumba hivyo pasipo kuchangisha fedha kwa wananchi.

Kukamilika kwa ujenzi wa madarasa hayo 152 yaliyojengwa kwa shilingi 3,040,000,000 kunaifanya Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kumaliza tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa kwa shule za Sekondari.




# Miaka 61 ya Uhuru, Sengerema Yajivunia kwa Maendeleo

Wananchi wilayani Sengerema mkoani Mwanza wametakiwa kujivunia kwa maendeleo yaliyopatikana wilayani humo ukilinganisha na kabla ya uhuru ambapo kulikuwa na changamoto nyingi za kimaendeleo.

Hayo yameelezwa leo na Mkuu wa Wilaya ya Sengerema Mhe. Senyi Ngaga wakati wa maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru yaliyofanyika sekondari ya Sengerema ambapo pia yameenda sambamba na kongamano la wazi lililowashirikisha viongozi mbalimbali wa serikali, madhehebu ya dini, wazee maarufu na wananchi wa Sengerema.

Mhe. Ngaga amesema kabla ya Uhuru Wilaya ya Sengerema haikuwa na shule ya sekondari lakini kwa sasa kuna shule za sekondari 43, shule za msingi zilikuwa 22 lakini kwa sasa kuna shule za msingi 110.

Ameongeza kusema Serikali imeendelea kutekeleza miradi mikubwa ikiwemo ile ya sekta za Nishati, Maji, afya, barabara na maendeleo ya jamii.

"Tunayo miradi mingi mikubwa ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa nchini kote, ikiwemo ndani ya Wilaya yetu, ikiwemo daraja la Busisi, daraja hili likikamilika litapunguza kero nyingi, haya ndiyo maendeleo tuliyokuwa tunatafuta baada ya kupata uhuru, tuna kila sababu ya kumpongeza Mhe Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan." amesisitiza Mhe. Ngaga.

Meneja wa wakala wa Barabara za vijijini na mijini (TARURA) Wilaya ya Sengerema mhandisi Prosper Francis amesema kabla ya uhuru Wilaya ya Sengerema haikuwa na mtandao wa barabara unaoeleweka bali kulikuwa na njia ndogo ndogo za waenda kwa miguu lakini kwa sasa Wilaya Sengerema ina mtandao wa barabara zenye urefu wa kilomita 2,709.

Meneja Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilaya ya Sengerema Mhandisi Musa Bujiku amesema hapo awali maji katika mji wa Sengerema yalikuwa yanatoka kwa mgao kwa sasa Wilaya inajivunia kwa kupata miradi mingi ya maji ambapo amesema kwa mwaka huu wa fedha serikali imetoa kiasi cha bilioni 47 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maji ambayo inatarajiwa kukamilika mwaka 2023 ambapo upatijanaji wa maji vijijini utapanda kutokana asilimia 57 asilimia 85.

Maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru yamefanyika Sekondari ya Sengerema na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali na madhehebu ya dini pamoja na wananchi.



# Sengeremaa Kuongeza Uzalishaji wa Zao la Pamba

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Adam Kigoma Malima amewaagiza wataalamu wa kilimo waliopo katika Halmashauri zote za Mkoa wa Mwanza kuhakikisha wanatoa elimu ya kutosha kwa wakulima wa zao la Pamba waliopo mkoani wa namna bora ya uzalishaji wa zao hilo hili kuongeza uzalishaji kutoka kilo 150 za sasa hadi kufikia kilo 500 hadi 600 kwa hekari moja.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza ametoa agizo hilo wakati akizindua msimu wa upandaji wa zao la Pamba uliofanyika kata ya Nyapande na kuhudhiriwa na viongozi mbalimbali wa Mkoa, Wilaya pamoja na wakulima.

Amesema Maafisa ugani waliopo katika halmashauri zote wanatakiwa kuhakikisha wanawatambua wakulima wa mfano wa zao la Pamba waliopo katika maeneo yote ya Wilaya za Mkoa wa Mwanza ili waweze kuwapatia elimu bora ya kilimo cha zao la Pamba kuanzia hatua ya upandaji hadi kuvunwa kwake.

"Mimi ninataka kuanzia msimu huu, uzalishaji wa Pamba uwe wa wastani wa kilo 500 hadi 600 kwa hekari 1 na si kilo 150 kama ilivyo, ninyi maafisa ugani ndio wa kutoa elimu juu ya kilimo chenye tija kwa wakulima wote wa zao la Pamba hususani kwa wale wakulima wa mfano" alisema Mhe. Malima.

Sambamba na hilo Mhe. Malima ameziagiza Halmashauri zote za Mkoa wa Mwanza kuanzisha mashamba darasa ya Wilaya ili wakulima wote wa zao hilo wajifunze kwa vitendo.

Mbunge wa jimbo la Sengerema Mhe.Hamis Tabasamu amempongeza Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa shilingi bilioni 150 za ruzuku ya mbolea kwa wakulima kote nchini hivyo amewataka wananchi wote kuchangamkia fursa hiyo.

Mhe.Tabasamu pia amemwomba Mkuu wa Mkoa wa Mwanza kuhakikisha serikali inawachukulia sheria kali wauzaji wa pembejeo feki ili kukomesha tatizo hilo ambalo kwa sasa limekuwa ni tatizo sugu.

Mapema akitoa taarifa ya uzinduzi wa zoezi hilo kwa Mkuu wa Mkoa Afisa ugani ndugu Isack Shija amesema kwa sasa wataalamu wa kilimo wanasisitiza upandaji wa zao la Pamba unaotumia vipimo vya sentimita 60 msitari hadi msitari hadi mwingine na sentimita 30 shina moja hadi jingine ambapo hekari moja huweza kutoa miche 44,444 ambapo hapo hapo awali vipimo vilivyotumika vilikuwa ni sentimita 90 msitari mmoja hadi mwingine sentimita 40 shina hadi shina ambavyo viliweza kutoa miche 22,222 hivyo upandaji huu wa kisasa umeongeza tija kwa wakulima.

Msimu wa 2021/2022 Mkoa wa Mwanza ulifanikiwa kuzalisha tani 15,000 za zao la Pamba ambapo miongoni mwa hizo Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema ilifanikiwa kuzalisha tani 3,199 ya lengo la kuzalisha tani 5,150.

Kwa msimu wa 2022/2023 Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema inatarajia kuzalisha tani 5897 za Pamba.



# Zaidi ya Watoto 130,000 Sengerema Wapatiwa Chanjo ya Polio Awamu ya

Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema Mkoani ilizindua rasmi kampeni siku 4 ya utoaji wa Chanjo ya matone ya Polio awamu ya nne tarehe 1 Disemba 2022, ambapo jumla ya watoto 135,615 wenye umri chini ya miaka mitano walitarajiwa kupatiwa chanjo hiyo.

Akizindua kampeni hiyo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema Binuru Shekidele amewataka wazazi na walezi wote wenye watoto walio chini ya miaka mitano kuhakikisha watoto hao wanapatiwa chanjo ya matone ya Polio katika vituo vya kutolea huduma za afya na majumbani ambapo watoa huduma watapita.

"Suala la kupatiwa chanjo ya matone ya Polio si la hiari ni la lazima, hivyo wazazi na walezi hakikisheni watoto wenu wanapatiwa chanjo hii kinyume na hapo tutawachukulia hatua kali wazazi wote watakaoshindwa kuwapeleka watoto kupata chanjo kwani takwimu zote za watoto wenye sifa za kupatiwa Chanjo hii tunazo " alisisitiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri.

Aidha Mkurugenzi Mtendaji amewashukuru wazazi na walezi wote waliojitokeza kwa ajili ya chanjo hiyo ambapo amesema kwa kufanya hivyo ni kulisaidia taifa katika kupunguza magonjwa ambayo yanaweza kuzuilika.

Naye msimamizi wa chanjo ngazi ya Mkoa Dkt. Saula Beichumila amesema chanjo hiyo ya awamu ya nne kitaifa ni mhimu sana kwa watoto kwani ndiyo hutengeneza kinga mwilini ya ugonjwa wa Polio hivyo amesisitiza wazazi na walezi kuhakikisha watoto wenye sifa wanapatiwa chanjo hiyo.

Kampeni ya Chanjo ya Polio awamu ya nne ilizinduliwa kwenye kituo cha afya cha Sengerema ambapo Chanjo hii ilitolewa kwenye vituo vyote vya kutole huduma za afya na majumbani. Kampeni hii ilihitimishwa siku ya jumapili tarehe 04 Disemba, 2022.







## DC Sengerema Aongoaza Wananchi Kufanya Usafi Kituo cha Afya Sengerema

Picha mbalimbali kuhusu tukio la kufanya usafi kuelekea kwenye maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru tarehe 09 Disemba ambapo Mkuu wa Wilaya ya Sengerema Mhe. Senyi Ngaga aliongoza viongozi mbalimbali wa Wilaya pamoja na wananchi kufanya safi kwenye kituo cha afya Sengerema.

Akihitimisha zoezi hilo Mhe. Ngaga aliwashukuru wananchi wote waliojitokeza kufanya usafi kituoni hapo ambapo amesema zoezi la kufanya usafi lililofanyika leo ni mwendelezo wa matukio mhimu ambayo Wilaya imeamua kuyafanya kuelekea kwenye kilele cha maadhimisho ya miaka 61 Uhuru.

Mkuu wa Wilaya amewaribisha wananchi wote kwenye kilele cha maadhimisho hayo yalifanyika siku ya ijumaa tarehe 09.12.2022 Sekondari ya Sengerema ambapo kulikuwa na burudani mbalimbali pamoja na kongamano la miaka 61 ya Uhuru.




# Sengerema Yazindua Zoezi la Uapandaji Miti

Katika kuadhimisha miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara Wilaya ya Sengerema Mkoani Mwanza imezindua rasmi zoezi la upandaji wa miti lenye lengo kuhifadhi mazingira katika maeneo yote ya Wilaya.

Akizindua zoezi hilo ambalo limeandaliwa na Shirikisho la walimu ambao ni makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Sengerema Mkuu wa Wilaya ya Sengerema Mhe. Senyi Ngaga amewaagiza wananchi wote pamoja na taasisi zote zilizopo wilayani hapa kuhakisha zinapanda miti hususani ile ya matunda katika maeneo yao ili kuhifadhi mazingira na kuboresha afya.

"Tupandeni miti ili tukabiliane na haya mabadiliko ya tabia ya nchi, mwenendo wetu wa ukataji miti hauendi sambamba na upandaji wa miti, hivyo tuhakikishe tuapanda miti ili tuweke vizuri mazingira yetu" alisisitiza Mhe. Nganga.

Aidha Mhe. Nganga amesema lengo la Wilaya ni kupanda miti isiyopungua milioni moja na nusu kwa mwaka hivyo ni vyema kwa wananchi wote kuongeza kasi ya upandaji wa miti ili kufikia lengo hilo. Amesema katika kuadhimisha miaka 61 ya uhuru tarehe 9 Disemba 2022 pamoja na matukio mengine Wilaya ya Sengerema itaendeleza zoezi la upandaji wa miti kwa kushirikiana na TFS ili kifikia lengo la kupanda miti zaidi ya milioni moja na nusu kwa mwaka.

Mwenyekiti wa shirikisho la walimu ambao ni makada wa CCM Wilaya ya Sengerema Mwalimu Sylivesta Sama amesema wataendelea na zoezi la upandaji wa miti pamoja na uhifadhi wa mazingira katika maeneo yote ya Wilaya ya Sengerema ikiwemo barabara ya kutoka Busisi hadi Geita hivyo ameomba wananchi wa maeneo husika kuitunza ili isiharibiwe na mifugo.

Zoezi la upandaji wa miti limezinduliwa kwa kupanda miti zaidi ya 1,800 kwenye chuo cha VETA Sengerema.





# Sekondari Sengerema Zatakiwa Kushirikiana Kuinua Taaluma

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema Binuru Shekidele amezitaka shule za Sekondari zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kuhakikisha zinashirikiana katika kutatua changamoto mbalimbali ya kitaaluma kujifunza kutoka kwa shule zinazofanya vizuri ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.

Mkurugenzi Mtendaji ameyasema hayo wakati wa hafla ya kupokea matokeo ya mtihani wa kumaliza nwaka 2022 kwa kidato cha kwanza na cha tatu kwa shule za Sekondari zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema mtihani ambao umekuwa ukifanyika kila mwaka na kusimamiwa kwa Umoja wa Wakuu wa Shule (TAHOSA).

Mkurugenzi Mtendaji amesema kuna baadhi ya shule katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema imekuwa zikifanya vizuri kitaaluma na zingine zimekuwa zikifanya vibaya kila mwaka hivyo amewaagiza wakuu hao wa shule kuweka mipango mizuri ili kuondokana na matokeo mabaya kwa wanafunzi.

"Tuone namna nzuri ya kusaidiana kwenye baadhi ya masomo, kwanini shule zinazofanya vizuri ni zilezile na zinazifanya vibaya pia ni zilezile, tuchukue hatua tubadilke tunaweza na zile shule zinazofanya vibaya tutaziweka kwenye uangalizi maalumu"

Mwenyekiti wa kamati ya taaluma ya TAHOSA Mwalimu Christine Zegera akiwasilisha matokeo hayo amesema miongoni mwa changamoto zilizojitokeza katika kufanikisha mtihani huo ni pamoja na gharama ndogo za uendeshaji wa mtihani huo ukilinganisha na hali halisi ya gharama za maisha kwa sasa ambapo kumesababisha kamati ya maandalizi kushindwa kukidhi mahitaji ya huduma kwa walimu hasa kwa wale wanaotoka mbali na vituo vya kazi kupata chakula na malazi.

Mwenyekiti huyo amependekeza kwa mwaka ujao kila mtahiniwa achangiwe kiasi cha shilingi 5500 ili kukidhi gharama za uendeshaji wa mitihani hiyo.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Sekondari Amani Tangalo amesema kufanyika kwa mtihani huo inasaidia Halmashauri kuweza kujua ni maeneo yapi yawekewe mkazo zaidi na walimu na pia husaidia kupata picha halisi ya matokeo ya kidato cha pili na nne kwa mwaka unaofuata hivyo amewataka wakuu wa shule kuhakikisha wanakuwa na mikakati thabiti ili kuboresha taaluma katika shule husika.

Mtihani huo wa pamoja hufanyika kila mwaka ambapo hushirikisha kidato cha kwanza na cha tatu. Kwa mwaka huu jumla ya shule za Sekondari 40 zineshiriki katika mtihani huo kwa kidato cha kwanza na shule 38 zilishiriki kwa mtihani wa kidato cha tatu.

Katika matokeo hayo Seminari ya Sengerema Imeongoza katika shule 40 kwa kidato cha kwanza kwa kupata wastani wa alama 69.9 na shule ya Twitange imeongoza kwa kidato cha tatu katika shule 38 kwa kupata wastani wa alama 49.5.



# Dc Sengerema Akemea Utoro, Ahimiza Uandikishaji Wanafunzi Shuleni

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema Mhe. Senyi Ngaga ameitaka jamii kutokuwaachia walimu suala la utoro mashuleni na uandikishishaji wanafunzi wa awali na darasa la kwanza badala yake ameitaka jamii yote kuwajibika ili kukomesha utoro na kufikia lengo la uandikishaji wanafunzi wa awali na darasa la kwanza.

Mhe. Ngaga ametoa agizo hilo ijumaa Disemba 16, 2022 kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya cha kujadili taarifa ya kipindi cha Julai hadi Disemba 2022 kikao kilichofanyika Sekondari ya Sengerema.


Amesema kumekuwa na tabia ya baadhi ya viongozi wa vijiji na kata kuwaachia walimu kwenye ufuatiliaji wa utoro na wanafunzi wanaotakiwa kuandikishwa elimu ya awali na darasa la kwanza kitu ambacho si sahihi na badala yake amewataka viongozi pamoja na wananchi washirikiane ili kufikia malengo ya sekta ya elimu.

"Kinachotokea sasa hivi watoto wote tumewaachia walimu, ndiyo changamoto kubwa iliyopo, kila mtu akijua nafasi yake na akatimiza wajibu hili jambo tunaweza kulitatua" amesema Mhe. Ngaga.

Katika hatua nyingine Mhe. Ngaga amewataka watendaji wote kuhakikisha wanatumia miongozo ya Elimu iliyopo ili kukomesha tabia ya wanafunzi wengi wa kidato cha kwanza ambao wamekuwa hawaripoti mashuleni hivyo amewataka watendaji kusimamia suala hilo sambamba na uhamasishaji wa uandikishaji wa watoto wenye umri wa kwenda shule za awali na darasa la kwanza uandikishaji ambao umeanza tangu mwezi Oktoba na utafungwa tarehe 31 Disemba 2022.

"Suala la utoro linahitaji mkakati wa pamoja, tutumie miongozo na sheria zilizopo tutafanikiwa, kwani utoro unaathiri si tu ufundishaji bali hata taaluma" ameshauri Mwalimu Benson Mpanju ambaye ni Afisa Elimu kata ya Buzilasoga.

Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi Ndugu Donati Bunonosi amesema kwa upande wa watoto wenye umri wa kwenda shule (maoteo) kwa elimu ya awali ni 10,859 ambao wamekwisha andikishwa hadi sasa ni watoto 9,563 sawa na asilimia 88.07 ya lengo na darasa la kwanza wanaotakiwa kuandikishwa ni 10,765 walioandikishwa hadi sasa ni watoto 9,689 sawa na asilimia 90 ya wanafunzi wanaotakiwa kuandikishwa.



# Sengerema Yaunda Jukwaa la Wadau Kilimo Bora cha Maharage

Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza imeanzisha Jukwa la wadau wa kilimo bora cha Maharage ambalo litakuwa na jukumu la kuwaunganisha wakulima, serikali, na wadau wengine ili kuendeleza kilimo cha zao hilo.

Mratibu wa shirika la Matumaini Mapya ambalo linajihusisha na umasishaji wa kilimo cha zao hilo nchini Tanzania Dkt. kaserwa Bigirwa amesema lengo la kuanzisha Jukwaa hilo ni pamoja na kuhamasisha na kuelimisha wakulima juu ya kilimo bora cha Maharage, pamoja na kuimarisha mitandao ya wakulima wa maharage kuanzia ngazi ya wilaya hadi Taifa.

"Tanzania inaongoza kwa uzalishaji wa zao la Maharage lakini mkulima anakabiliwa na changamoto kadhaa za uzalishaji wa zao hilo ikiwemo uelewa mdogo wa kuendesha kilimo bora, mabadiliko ya tabia nchi pamoja na ukosefu wa masoko ya uhakika" alisema Dkt. Kaserwa.

Dkt. Kaserwa ameongeza kusema kuwa kuanzishwa kwa Jukwaa hilo kutasaidia wakulima kupata taarifa za kilimo kutoka kwa wataalamu na taasisi mbalimbali zinazojihusika katika mnyororo wa thamani wa kilimo kama vile watafiti, masoko ya mazao, bei, wauzajiwa pembejeo pamoja na wasafirishaji.

Kwa upande wa wakulima wanaojihusisha na zao la Maharage Wilayani Sengerema wameomba shirika hilo kwa kushirikiana na wadau wengine kuhakikisha wanawezesha wakulima juu ya elimu ya kilimo bora cha zao hilo la Maharage ili waondokane na kilimo cha mazoea ikiwemo kuchanganya mazao shambani.

"Tatizo kubwa tulilonalo sisi wakulima ni kuchanganya mazao mengi hasa Maharage na mengine, tusaidieni elimu tuachane na haya mazoea" alishauri ndugu Kazimili Chemu ambaye ni mkulima wa Maharage kutoka Nyantukara.

Jukwaa hilo lilimchagua ndugu Mikaeli Kazungu kuwa mwenyekiti na Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kuwa katibu wa jukwaa hilo.

# Habari Katika Picha



DC Sengerema Asisisitiza Upandaji wa miti ya Matunda katika Taasisi zote za Serikali



Chanjo ya Polio Awamu ya nne





Uzinduzi wa Msimu wa Upandaji wa Pamba 2022

# Habari Katika Picha




Sekondari ya Nyamatongo

Wajumbe wa ALAT Mkoa wa Mwanza Wakagua Miradi Sengerema

Jengo la Dharula Hospitali ya Wilaya



## Miaka 61 YA Uhuru



# Salamu za Sikukuu ya Krismasi 2022




# Uandikishaji wa Wanafunzi Awali na Darasa la Kwanza



# Fomu za Kujiunga na Kidato cha Kwanza 2023




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA
HAFLA YA MAKABIDHIANO YA VYUMBA VYA MADARASA 152 NYAMPULUKANO SEKONDARI
28/12/2022
"Mtoto ukichaguliwa kujiunga kidato cha kwanza ukaacha huu ni uhujumi uchumi, Serikali imewekeza kwenye hizi shule, madarasa na madawati yapo kwa ajili yenu, mwaka huu tutatoa mfano kwa watoto wote watakao acha kujiunga kidato cha kwanza 2023"
MHE. SENYI NGAGA
MKUU WA WILAYA YA SENGEREMA
Tufuatilie
sengeremadc
http://www.sengeremadc.go.tz/

# Salamu za Mwaka Mpya 2023

